# AZIMIO LA IMANI



Imekusanywa Na Aimee Semple McPherson

# AZIMIO LA IMANI

Imekusanywa Na Aimee Semple McPherson

Kitabu hiki kimetumia Biblia Takatifu fafsiri ya Word*Project* ispokuwa pale tu ambapo imeelezwa vinginevyo.

Hili Azimio la Imani lilikusanywa mwanzoni na Aimee Semple McPherson, linaweka wazi mbele yako nguzo za msingi na linashirikisha hatua nne muhimu za kanisa la Foursquare za kumuwasilisha Yesu Kristo kama:

Mwokozi wa ulimwengu

Ubatizaye kwa Roho Mtakatifu

Mponyaji wa magonjwa yetu

Mfalme wa wafalme ajaye na Bwana wa mabwana.

Imetafsiriwa kwa Kiswahili na Gabriel Baraza Njakusi.
Imehaririwa na Stacy Collins.

Kwa taarifa zaidi kuhusu familia ya Foursquare tembelea tovuti www.foursquare.org au piga simu ya bure 1-888-635-4234.

Imechapishwa na Foursquare Missions Press © 2005.

FMP
Foursquare Missions Press

# YALIYOMO

Azimio la Imani linalofungamana na:

| | | |
|---|---|---|
| I. | MAANDIKO MATAKATIFU | 4 |
| II. | UTATU MTAKATIFU WA MILELE | 5 |
| | Mungu Baba | |
| | Mungu Mwana | |
| | Mungu Roho Mtakatifu | |
| III. | ANGUKO LA MWANADAMU | 8 |
| IV. | MPANGO WA UKOMBOZI | 9 |
| V. | WOKOVU KWA NJIA YA NEEMA | 10 |
| VI. | TOBA NA KUKUBALIWA | 11 |
| VII. | KUZALIWA UPYA | 12 |
| VIII. | MAISHA YA KIKRISTO YA KILA SIKU | 13 |
| IX. | UBATIZO WA MAJI NA MEZA YA BWANA | 14 |
| X. | UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU | 16 |
| XI. | MAISHA YALIYOJAWA NA ROHO | 17 |
| XII. | VIPAWA NA TUNDA LA ROHO | 19 |
| XIII. | KIASI | 20 |
| XIV. | UPONYAJI WA KIMUNGU | 21 |
| XV. | KUJA KWA YESU MARA YA PILI | 22 |
| XVI. | MAHUSIANO YA KANISA | 23 |
| XVII. | SERIKALI YA KIRAIA | 25 |
| XVIII. | HUKUMU | 26 |
| XIX. | MBINGU | 26 |
| XX. | JEHENAMU | 28 |
| XXI. | UINJILISTI | 29 |
| XXII. | ZAKA NA MATOLEO | 31 |



# I. MAANDIKO MATAKATIFU

Tunaamini kwamba Biblia Takatifu ni Neno la Mungu aliye hai, asiye badilika, imara, na kigeugeu kama mwandishi wake, Bwana Yehova, kwamba iliandikwa na watu watakatifu wa kale walioongozwa na kuvuviwa na Roho Mtakatifu, kwamba ni taa iliyowashwa kuongoza miguu ya ulimwengu uliopotea katika kina kirefu cha dhambi na masikitiko, ili kuuleta ulimwengu katika kilele cha haki na utukufu, kioo kisichokuwa na mawingu kinachofunua uso wa mwokozi aliyesulubiwa, timazi ya kunyoosha maisha ya kila mtu na jamii, upanga wenye makali ukatao kuwili unao sababisha mtu atambue dhambi zake na matendo maovu, Kamba iliyosokotwa yenye nguvu ya upendo na laini kuvuta wenye dhambi kwa Kristo Yesu, mafuta laini yawezayo kulainisha na kuponya ya Giliedi, iliyopuliziwa pumzi ya Roho Mtakatifu iwezayo kuponya na kuinua kila tone la moyo ulioinama, msingi pekee wa ushirika wa Kikristo na umoja, wito wenye upendo wa Mungu wa pekee mwenye upendo wa milele, onyo ambalo linahitaji kuzingatiwa, muungurumo wa mbali wa upepo wa ghadhabu adhabu ya itakayowakuta watu wasiotilia maanani neno la Mungu, bango linaloelekeza mbinguni, ishara ya hatari ionyonya kutoka kuzimu, mamlaka ya juu ya kiungu na mahakama ya milele ambayo kwa viwango vyake watu, mataifa, na nguzo/ imani zote (dini zote) na nia watahukumiwa.

## Rejea ya Maandiko

> ...mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe. **Mathayo 24:35**

> Ee Bwana, neno lako lasimama Imara mbinguni hata milele. **Zaburi 119:89**

Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema. 2 Timotheo 3:16-17

Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu. Zaburi 119:105

Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu. Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu. 2 Petro 1:19-21

Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Yohana 5:39

Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.
2 Timotheo 2:15 ... Lakini, hapo tulipofika na tuenende katika lilo hilo. Wafilipi 3:16 (Pia, 1 Yohana 4:1; Isaya 8:20; 1 Wathesalonike 5:21; Matendo ya Mitume 17:11; 1 Yohana 4:6; Yuda 3; Waefeso 6:17; Zaburi 119:59-60; Wafilipi 1:9-11)



## II. UTATU MTAKATIFU WA MILELE

Tunaamini kwamba yuko Mungu mmoja pekee aishie na wa kweli, Muumba wa mbingu na nchi na vitu vyote vilivyomo, Alfa na Omega aliyekuwepo, aliyepo, na atakaye kuwepo, asiye kuwa na mwisho, amina, kwamba Yeye ni Mtakatifu na wa pekee, asiyekuwa na mwisho, mwenye nguvu, mpole, mwenye huruma, upendo na utukufu; anayestahili upendo wote na heshima, na wa kuaminiwa na utii,

mwenye mamlaka ya kutawala na nguvu, sasa na hata milele; na kwamba katika ushirika wa uungu wako watatu wanao lingana katika ukamlifu wa kiungu wanaotekeleza kazi tofauti lakini kwa kushirikiana katika ofisi zao katika kazi kuu ya ukombozi.

**Baba** – Ambaye utukufu wake unangaa sana kiasi kwamba mwanadamu hawezi kuutazama uso wake na akaishi, lakini ambaye moyo wake ulijawa na upendo na huruma kwa ajili ya watoto wake waliopotea katika dhambi, ya kwamba Alimtoa Mwanawe wa pekee bure kukomboa na kuwapatanisha kwake Mwenyewe.

**Mwana** – Aliye pamoja na Baba na wa milele pamoja na Baba, ambaye alichukuliawa mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu na kuzaliwa na bikira Mariamu, akatwaa namna ya mwanadamu, akazichukua dhambi zetu, akayabeba masikitiko yetu na kumwaga damu yake ya thamani katika msalaba wa Kalvari alinunua ukombozi kwa ajili ya wote ambao wangemwamini kisha akakata vifungo vya mauti na kuzimu akafufuka kutoka kaburini na akapaa juu na kuteka mateka, kwamba kama mpatanishi mkuu kati ya Mungu na mwanadamu asimame mkono wa kuume wa Baba akiombea wote ambao aliotoa uhai wake kwa ajili ya maisha yao.

**Roho Mtakatifu** – Nafsi ya tatu katika Utatu Mtakatifu ni Roho wa Baba mwenye nguvu zote, aliyeko kila mahali, anayefanya kazi isiyokuwa na lugha sahihi ya kutumia kwa kuelezea utume wake hapa duniani, anayesababisha watu wajue dhambi zao, haki na hukumu, akiwavuta wenye dhambi waje kwa Mwokozi, anaye kemea, anaye sihi kwa hisia, anaye tafuta, anaye fariji, anaye harakisha, anaye fundisha, anaye tukuza, abatizaye na kuwavika uweza utokao juu wale

wanaoitikia huduma yake ya huruma akiwaandaa kwa ajili ya siku kuu ya ujio wa Bwana.

## Rejea ya Maandiko

> ...kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwapo mwingine. Isaya 43:10

> ...Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba; mimi sijui mwingine. Isaya 44:8

> Kisha akasema, Huwezi kuniona uso wangu, maana mwanadamu hataniona akaishi. Kutoka 33:20

> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16

> Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika. Yohana 1:1-3 (Pia, Ayubu 38:4-7)

> Tazama, bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake Imanueli; Yaani, Mungu pamoja nasi. Mathayo 1:23

> Mimi, naam, mimi, ni Bwana, zaidi yangu mimi hapana mwokozi. Isaya 43:11

> Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu; ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira yake. 1 Timotheo 2:5-6

> Kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja. Waefeso 2:18

> Kwa maana wako watatu washuhudiao mbinguni, Baba, na Neno, na Roho Mtakatifu, na watatu hawa ni umoja. 1 Yohana 5:7

> Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia. Yohana 15:26 (Pia, 1 Wakorintho 13:14; Mathayo 28:19; Warumi 8:11; Yohana 16:7-14).



## III. ANGUKO LA MWANADAMU

Tunaamini kwamba mtu aliuumbwa katika sura ya Mungu ambaye mbele zake alitembea katika utakatifu na usafi, lakini kwamba kwa hiari yake mwenyewe aliamua kutokutii na kukosea, aliianguka kutoka katika bustani ya Edeni, mahali pa usafi na kutokuwa na hatia, hadi kwenye kina kirefu cha dhambi na tabia chafu isiyokuwa ya kiMungu, na kwamba katika matokeo haya wanadamu wote ni wenye dhambi wameuzwa kuwa mali ya Shetani, wenye dhambi si kwa kulazimishwa bali kwa kuchagua wenyewe, awe chini ya mamlaka ya uovu na kukosa mamalaka ya kupata asili ya utakatifu huo unaotakiwa na sheria ya Mungu wamegeukia kutenda maovu, wenye hatia na bila kuwa na sababu yeyote ya kujitetea na kihalali wanastahili hukumu ya haki ya Mungu Mtakatifu.

### Rejea ya Maandiko

> Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mwanzo 1:27

> Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi... Warumi 5:12

> Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi... Warumi 5:19 (Pia, Yohana 3:6; Zaburi 51:5; Warumi 5:15-19, 8:7)

> ...Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe... Isaya 53:6 (Pia, Mwanzo 3:9-18, 6:12)

> ...ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine. Waefeso 2:3 (Pia, Warumi 1:18-32, 2:1-16; Mathayo 20:15; Wagalatia 2:10; Ezekieli 18:19-20)

...hata wasiwe na udhuru... **Warumi 1:20** ...ili kila kinywa kifumbwe, na ulimwengu wote uwe chini ya hukumu ya Mungu... **Warumi 3:19**



## IV. MPANGO WA UKOMBOZI

Tunaamini kwamba tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu, mwenye haki kwa wale wasio haki, bure, na kwa uteuzi wa kiungu wa Baba akichukua nafasi ya mwenye dhambi kwa kutwaa dhambi zake (mwenye dhambi), akipokea hukumu yake, akifa kifo chake, akilipa adhabu yake kikamilifu, akitia sahihi kwa damu ya maisha yake msamaha wa kila mmoja atakaye mwamini, kwamba kwa njia ya Imani na kukubali sadaka iliyonunuliwa katika mlima wa Kalvari, mwenye dhambi mbaya yeyote anaweza kusafishwa kwa uchafu wake na kufanywa mweupe kuliko theluji.

### Rejea ya Maandiko

Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. **Isaya 53:5**


...ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema. **Tito 2:14**

Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa. **Isaya 55:7**

Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee. **Waebrania 7:25**

Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji;

zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu. Isaya 1:18



## V. WOKOVU KWA NJIA YA NEEMA

Tunaamini kwamba wokovu kwa wenye dhambi ni kwa njia ya neema pekee, kwamba hatuna haki au wema wetu wenyewe ambao tunaweza kutafuta neema ya kiungu, lazima tuje na kujitupa katika rehema isiyoweza kushindwa na upendo wake yeye aliyetununua na kutuosha katika damu yake mwenyewe, tukisihi ukamilifu na haki ya Kristo Mwokozi, tukisimama juu ya neno lake na kukubali zawadi yake ya bure ya upendo na msamaha.

### Rejea ya Maandiko

Kwa maana mmeokolewa kwa neema... Waefeso 2:8

...Hakuna mwenye haki hata mmoja. Warumi 3:10

...kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu... Warumi 3:23

Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi; sisi sote twanyauka kama jani, na maovu yetu yatuondoa, kama upepo uondoavyo. Isaya 64:6

Amin, amin, nawaambia, Yeye aaminiye yuna uzima wa milele. Yohana 6:47

Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo. Waefeso 2:13

Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu. Warumi 6:23

## VI. TOBA NA KUKUBALIWA



Tunaamini kwamba juu ya toba ya dhati, huzuni ya kimungu kwa dhambi, na kukubalika kwa moyo wako wote wa Bwana Yesu Kristo, wale wanaomwomba wanaweza kuhesabiwa haki kwa imani, kupitia kwa damu yake ya thamani na kwamba badala ya hukumu waweze kupata amani iliyobarikiwa sana, uhakika na neema ya Mungu, kwamba kwa mikono wazi ya rehema na msamaha Mwokozi anasubiri kupokea kila mwenye dhambi anayekuja kwake kwa toba halisi na maombi ya rehema, anafungua mlango wa moyo wake na kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mfalme.

### Rejea ya Maandiko

Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.
1 Yohana 1:9

Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu. Warumi 5:1-2

Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Warumi 8:1

Uwajulishe watu wake wokovu, Katika kusamehewa dhambi zao. Kwa njia ya rehema za Mungu wetu, Ambazo kwa hizo mwangaza utokao juu umetufikia, Kuwaangaza wakaao katika giza na uvuli wa mauti, Na kuiongoza miguu yetu kwenye njia ya amani. Luka 1:77-79

Wote anipao Baba watakuja kwangu; wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe. Yonana 6:37



## VII. KUZALIWA UPYA

Tunaamini kwamba mabadiliko yanayotokea ndani ya moyo na maisha wakati wa kumgeukia Yesu ni ya uhalisia, kwamba mwenye dhambi hapo huzaliwa mara ya pili katika njia ya kiutukufu na mageuzi, kwamba mambo ya kale yanapita na mambo yote yanakuwa mapya, hivi kwamba vitu ambavyo vilikuwa vinatamaniwa sasa vinadharauliwa, wakati vitu ambavyo sasa vinachukiwa vinachukuliwa kuwa takatifu na mpendwa, na kwamba baada ya kupokea haki ya Mkombozi na kupokea Roho wa Kristo, hisia mpya, tumaini jipya, shauku ya kufanya mambo mapya, na kuwa na mtazamo mpya katika maisha, muda na umilele hujaza moyo uliooshwa kwa damu ili kwamba shauku yake sasa ni kuungama dhambi waziwazi na kumtumikia Bwana akitafuta daima mambo yale yaliyo juu mbinguni.

### Rejea ya Maandiko

...Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Yohana 3:3

Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya. 2 Wakorintho 5:17

Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia. Yohana 15:19

Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu. Wagalatia 2:20

...wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu; ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake,ili

aonyeshe haki yake ,kwa sababu ya kuziachilia katika ustahimili wa MUNGU dhambi zote zilzotangulia kufanywa.Warumi 3:24-25

Heri mtu yule asiyekwenda Katika shauri la wasio haki; Wala hakusimama katika njia ya wakosaji; Wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku. Zaburi 1:1-2



## VIII. MAISHA YA KIKRISTO YA KILA SIKU

Tunaamini kwamba baada ya kuoshwa na damu ya thamani ya Yesu Kristo na baada ya kupokea ushuhuda wa Roho Mtakatifu baada ya kumgeukia Yesu, ni mapenzi ya Mungu kwamba tujitakase kila siku na tuwe washirika wa utakatifu wake, tukikua wenye nguvu bila kushuka katika viwango vya imani, nguvu, maombi, upendo na huduma, kwanza kama watoto tutamani maziwa ya kweli ya neno la Mungu; kisha kama watoto wapendwao tutembee kwa unyenyekevu, tukitafuta kwa juhudi au kwa bidii maisha yaliyofichika, ambapo umimi unapungua na Kristo, anaongezeka kisha kama watu wenye nguvu waliovaa silaha zote za Mungu, wanaosonga mbele tukiteka maeneo mapya katika jina lake Kristo chini ya bendera yake iliyo pakwa damu yake, daima tukiishi maisha ya uvumilivu kiasi, maisha yasiyokuwa na ubinafsi, maisha ya kiungu ambayo yatakisi uhalisia wa Krisro aliyeko ndani yetu.

### Rejea ya Maandiko

Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati. 1 Wathesalonike 4:3

Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama,

wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. 1 Wathesalonike 5:23

Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu. 2 Wakorintho 7:1

Bali njia ya wenye haki ni kama nuru ing'aayo, Ikizidi kung'aa hata mchana mkamilifu. Methali 4:18

Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na imani kwa Mungu... Waebrania 6:1

Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho. Warumi 8:5

Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia, nayo itaitwa, Njia ya utakatifu; wasio safi hawatapita juu yake; bali itakuwa kwa ajili ya watu hao; wasafirio, wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo. Isaya 35:8 (Pia, 1 Petro 2:2)



## IX. UBATIZO WA MAJI NA MEZA YA BWANA

Tunaamini kwamba ubatizo wa maji mengi kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, kulingana na agizo la Bwana, ni ishara ya nje ya baraka ya kazi ya ndani, ni alama ya kipekee na nzuri inayotukumbusha ya kwamba Bwana alitufia katika msalaba wa Kalvari, tunajihesabu sisi wenyewe kwamba tumekufa kwa habari ya dhambi, na utu wetu wa kale uligongemelewa misumari katika mti pamoja Naye; na kwamba kama vile alivyoshushwa mtini na kuzikwa, vivyo hivyo tumezikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti: kwamba kama vile Kristo alivyofufuliwa kutoka kwa wafu na utukufu wa Baba, vivyo hivyo tunatakiwa kutembea katika upya wa uzima.



Tunaamini katika kukumbuka na kusherehekea meza ya Bwana kwa kutumia njia takatifu ya mkate uliomegwa, ni aina ya Mkate wa thamani wa Uzima, hata Yesu Kristo, ambaye mwili wake ulijeruhiwa kwa ajili yetu, na kwa njia ya kinyaji cha mzabibu, ni aina fulani iliyobarikiwa ambayo daima inatukumbusha ushiriki wa damu ya Mwokozi iliyo mwagika, aliye mzabibu wa kweli na ambaye watoto wake ndio matawi; ya kwamba sherehe hii ni upinde wa mvua wenye utukufu uliopo katikati ya miaka kuanzia Kalvari na kurudi kwa Bwana, wakati ambapo katika ufalme wa Baba, atashiriki mzabibu mpya na watoto wake na kwamba katika kushirikisha na kupokea sakramenti takatifu hii lazima utangulie na watu kujichunguza mioyo yao, wajipime, msamaha na upendo kwa watu wote, ya kwamba mtu yeyote asishiriki isivyo halali na kuinywea hukumu ya nafsi yake.

## Rejea ya Maandiko

Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu... Mathayo 28:19 (Pia, Matendo ya Mitume 2:37-38; Wagalatia 3:27-28)

Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Warumi 6:4 (Pia, Wakolosai 2:12; 1 Petro 3:20-21; Matendo ya Mitume 22:16)

Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu. Matendo ya Mitume 2:41 (Pia, Mathayo 28:19-20)

Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. 1 Wakorintho 11:26

Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe. 1 Wakorintho 11:28

Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? 2 Wakorintho 13:5



## X. UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU

Tunaamini kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ni ujio wa Mfariji tuliyeahidiwa katika nguvu na utukufu ulio kamili ili kumvika mwamini na uweza utokao juu kutukuza na kumwinua Bwana Yesu, kunena kwa kuvuviwa katika kushuhudia kuhusu yeye (Yesu), kukuza roho ya maombi, utakatifu, kuwa na kiasi, kumwezesha mwamini na kanisa kwa kivitendo, ubora, shangwe, kuwaleta watu kwa Yesu kwa nguvu za Roho Mtakatifu katika hali ya maisha tunayoishi na kwamba hii ikiwa bado matokeo ya mgawo wa Roho Mtakatifu, mwamini anaweza akawa na kila sababu ya kutarajia ujio wake (Roho Mtakatifu) kwa mfano kama ule aliokuja juu ya Wayahudi na watu wa Mataifa katika zile siku za Biblia na kama ilivyoandikwa katika neno la Mungu, ya kwamba inawezkana kwa kweli kusema juu yetu kama ilivyosema juu ya nyumba ya Kornelio Roho Mtakatifu alishuka juu yao kama na kwetu hapo mwanzo.

### Rejea ya Maandiko

Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu. Yohana 14:16-17

...ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache. Basi

walipokutanika, wakamwuliza, wakisema, Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme? Akawaambia, Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi. **Matendo ya Mitume 1:5-8**

Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka. **Matendo ya Mitume 2:4**

Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. **Matendo ya Mitume 8:17**

Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno. Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu. **Matendo ya Mitume 10:44-46**

Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri. **Matendo ya Mitume 19:6**

Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? **1 Wakorintho 3:16**



## XI. MAISHA YALIYOJAWA NA ROHO

Tunaamini kwamba wakati Roho Mtakatifu ni kama upepo wa nguvu uendao kwa kasi na kama ndimi za miale iliyo hai ambayo inaweza kutikisa na kuwasha moto jamii zote zije kwa Mungu, Yeye pia ni kama hua mpole, ahuzunishaye kwa urahisi na kujeruhiwa na ile hali ya kukosa heshima kwa Mungu, hali ya kuwa baridi (bila huruma), mazungumzo mabaya, majivuno,

roho ya kuhukumu na kulaumu, mawazo na matendo yasiyomheshimu Bwana Yesu, kwamba kwa hiyo, ni mapenzi ya Mungu kwamba tuishi na kutembea katika Roho kila wakati chini ya damu ya thamani ya Mwana-Kondoo, kutembea katika njia iliyo sahihi kwa unyoofu kama ka niguu ambayo haijafunikwa mbele za Mfalme, kuwa wavumilivu, mwenye upendo, kuwa wakweli, kutokuwa wanafiki, wenye maombi, wasio na manunguniko, kuwa tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa, kumtumikia Bwana.

## Rejea ya Maandiko

Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi. Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi. Waefeso 4:30-32


...kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote... Waefeso 6:18

Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu. Warumi 12:1-2

Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda. 1 Yohana 2:6

Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Wagalatia 5:16

Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi. 1 Wakorintho 3:17



## XII. VIPAWA NA TUNDA LA ROHO

Tunaamini kwamba Roho Mtakatifu ana vipawa vifuatavyo kumimina juu ya kanisa liaminilo la Bwana Yesu Kristo: hekima, maarifa, imani, uponyaji, miujiza, unabii, kupambanua, aina za lugha, kufasiri, kwamba kulingana na kiwango cha neema na imani alichonacho mpokeaji, vipawa hivi vimegawiwa kwa kila mtu kwa njia ya kipekee kama Roho Mtakatifu apendavyo, ya kwamba vinatakiwa na kutamaniwa kwa shauku kubwa katika mpangalio na kwa kiasi ambacho vinaonekana kuthibitisha na kubadilisha maisha ya mtu au watu kwa manufaa ya kanisa na kwamba tunda la Roho ni: upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, wema, imani, unyenyekevu, kiasi yanatakiwa yaonekane, yapaliliwe, na yalindwe kwa bidii kama mapambo ya matokeo ya kujazwa Roho Mtakatifu, kama ushaidi wa wazi na usioweza badilika na ama usioweza kukataliwa wa maisha yaliyojawa na Roho.

### Rejea ya Maandiko

Basi, ndugu zangu, kwa habari ya karama za roho, sitaki mkose kufahamu... Takeni sana karama zilizo kuu. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora. **1 Wakorintho 12:1, 31**

...lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye. **1 Wakorintho 12:11**

Vivyo hivyo na ninyi, kwa kuwa mnatamani sana kuwa watu wenye karama za roho, takeni kwamba mzidi sana kuwa nazo ili kulijenga kanisa. **1 Wakorintho 14:12**

Kwa sababu karama za Mungu hazina majuto, wala mwito wake. **Warumi 11:29**

Basi kwa kuwa tuna karama zilizo mbalimbali, kwa kadiri ya neema mliyopewa; ikiwa unabii, tutoe unabii kwa kadiri ya

imani; ikiwa huduma, tuwemo katika huduma yetu; mwenye kufundisha, katika kufundisha kwake; mwenye kuonya, katika kuonya kwake; mwenye kukirimu, kwa moyo mweupe; mwenye kusimamia kwa bidii mwenye kurehemu, kwa furaha. Warumi 12:6-8

Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu. Yohana 15:8

Na sasa hivi shoka limekwisha kuwekwa penye mashina ya miti; basi kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni. Luka 3:9



## XIII. KIASI

Tunaamini kwamba kuwa na kiasi katika maisha ya mwamini, ni jambo ambalo linabibi lijulikane na watu wote, kwamba uzoefu wake na mwenendo wa maisha ya kila siku kamwe visimwongoze kwenda mbali katika ile hali ya kutokuwa na kiasi, itikadi kali, madhihirisho yasiyokuwa mazuri, masengenyo, manunguniko, lakini kwamba kijitambua kwake, si mwepesi kuchukua hatua bila kufikiria, wenye usawa, mwororo, mwenye kusamehe, na uzoefu wa Kikristo wenye bidii, inapaswa kuwa moja kati ya uwiano thabiti, mtaratibu, mnyeneykevu, mwenye kujithabihu, na kufanana na sura na tabia ya Kristo.

### Rejea ya Maandiko

Upole wenu na ujulikane na watu wote. Bwana yu karibu. Wafilipi 4:5

...ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Waefeso 4:14-15

...haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya... 1 Wakorintho 13:5

Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi. Wakolosai 3:12-13



## XIV. UPONYAJI WA KIMUNGU

Tunaamini kwamba uponyaji wa kimungu ni uweza wa Bwana Yesu Kristo kuponya wagonjwa na wenye mateso kama jibu la maombi ya aminiye, kwamba yeye aliye yule jana, leo na milele hajawahi kubadilika lakini bado ni msaada ujitoshelezao wakati wa mateso, awezaye kukutana na mahitaji ya watu, na kuharakisha miili katika upya wa uzima, sawa na nafsi na roho kama jibu kwa imani ya wale waombao na kujitiisha chini ya mapenzi ya utawala wake wa kimungu.

### Rejea ya Maandiko

...Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, Na kuyachukua magonjwa yetu. Mathayo 8:17

Kwa maana rahisi ni lipi, ni kusema, Umesamehewa dhambi zako, au ni kusema, Ondoka, uende? Mathayo 9:5

Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. Marko 16:17-18

Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao; ukawajalie watumwa wako kunena neno lako kwa ujasiri wote, ukinyosha mkono wako kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa jina la Mtumishi

wako mtakatifu Yesu. Matendo ya Mitume 4:29-30

Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa. Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii. Yakobo 5:14-16



## XV. KUJA KWA YESU MARA YA PILI

Tunaamini kwamba kuja kwa Yesu mara ya pili ni ya kibinafsi na inakaribia sana, kwamba atashuka kutoka mbinguni na mawingu ya utukufu na sauti ya malaika mkuu na tarumbeta ya Mungu: na kwamba kuhusu saa hii hakuna mtu aijuae, waliokufa katika Kristo watainuka, kisha wale waliokombolewa ambao bado wako hai watanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, kumlaki Bwana angani, na kwamba watakuwa na Bwana milele; kwamba pia kwa Bwana miaka elfu moja ni kama siku moja, na kwamba hakuna mtu aijuae saa ya kurudi kwake, ambayo tunaamini imekaribia, tunapaswa kuishi kila siku kana kwamba anatarajiwa kuonekana na kurudi wakati wowote, kwa utii wa agizo lake lililo hai, "Nifanyie kazi mpaka nitakapokuja," kazi ya kuineza injili, kutuma wamishonari, na majukumu mengine kwa ujumla ya kulijenga kanisa yaendelezwe kwa juhudi na kwa uangalifu wa hali juu kana sio yetu wala kizazi kijacho hatufai kuishi katika mwili ili kuiona siku ya utukufu.

### Rejea ya Maandiko

Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya

Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.
1 Wathesalonike 4:16-17

...nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa; tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu... Tito 2:12-13

Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake... Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu... Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja. Mathayo 24:36, 42, 44

...kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu. Waebrania 9:28

...akawaambia, Fanyeni biashara hata nitakapokuja. Luka 19:13

Viuno vyenu na viwe vimefungwa, na taa zenu ziwe zinawaka; nanyi iweni kama watu wanaomngojea bwana wao, atakaporudi kutoka arusini, ili atakapokuja na kubisha, wamfungulie mara. Heri watumwa wale, ambao bwana wao ajapo atawakuta wanakesha. Amin, nawaambieni, atajifunga na kuwakaribisha chakulani, atakuja na kuwahudumia. Luka 12:35-37



## XVI. MAHUSIANO YA KANISA

Tunaamini kwamba baada ya kumkubali Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi na Mfalme, na baada ya kuzaliwa katika familia na mwili usionekana au kanisa la Bwana, ni wajibu mtakatifu wa mwamini, wakati wowote huu uko ndani ya uwezo wake, kujitambulisha, na kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya kujenga ufalme wa Mungu na kanisa la Kristo linaloonekana

hapa duniani, na kwamba kanisa kama hilo linaloonekana ni mkusanyiko wa waaminio, ambao wajiungamanisha pamoja katika ushirika wa Kikristo na katika umoja wa Roho, wakitunza sherehe za Kristo, wakimwabudu katika uzuri wa utakatifu, wakisemezana kwa zaburi na nyimbo na tenzi za rohoni, wakisoma na kutangaza Neno Lake, wakifanya kazi ya kuokoa roho, wakitumia njia mbalimbali kuendeleza kazi yake, wakikuza roho, wakitia moyo, wakiimarishana katika imani iliyo takatifu sana, na kufanya kazi kwa kushirikiana pamoja kama watoto wapendwao walio wengi lakini wa mwili mmoja ambao Kristo ndiye kichwa.

## Rejea ya Maandiko

Haleluya Nitamshukuru Bwana kwa moyo wangu wote, Barazani pa wanyofu wa moyo na katika mkutano. Zaburi 111:1

...tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia. Wabrania 10:24-25

...Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa. Mitume 2:47

Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake. Warumi 12:5 (Pia Warumi 12:6-8)

Ndipo wale waliomcha Bwana waliposemezana wao kwa wao. Naye Bwana akasikiliza, akasikia; na kitabu cha ukumbusho kikaandikwa mbele zake, kwa ajili ya hao waliomcha Bwana, na kulitafakari jina lake. Nao watakuwa wangu, asema Bwana wa majeshi, katika siku ile niifanyayo; naam, watakuwa hazina yangu hasa; nami nitawaachilia, kama vile mtu amwachiliavyo mwanawe mwenyewe amtumikiaye. Malaki 3:16-17



## XVII. SERIKALI YA KIRAIA

Tunaamini kwamba serikali ya kiraia ni uteuzi wa kiungu, kwa faida na mpangilio mzuri wa jamii ya wanadamu, na kwamba viongozi na watawala wanastahili kuombewa, kuwatii, na kuheshimiwa muda wote isipokuwa katika mambo yanayopinga mapenzi ya Bwana wetu Yesu Kristo, aliyemtawala wa dhamiri za watu, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

### Rejea ya Maandiko

...ila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo umeamriwa na Mungu. Hivyo amwasiye mwenye mamlaka hushindana na agizo la Mungu; nao washindanao watajipatia hukumu. Kwa maana watawalao hawatishi watu kwa sababu ya matendo mema, bali kwa sababu ya matendo mabaya. Basi, wataka usimwogope mwenye mamlaka? Fanya mema, nawe utapata sifa kwake... Warumi 13:1-3 (Pia, Kumbukumbu 15:18, 2 Samweli 23:3, Kutoka 18:21-23, Yeremia 30:21)

...Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu. Matendo ya Mitume 5:29

Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanum. Mathayo 10:28 (Pia, Danieli 3:15-18; Danieli 6:7-10; Matendo ya Mitume 4:18-20)

Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo. Mathayo 23:10

Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME, NA BWANA WA MABWANA. Ufunuo wa Yohana 19:16 (Pia, Zaburi 72:11, Warumi 14:9-13)



## XVIII. HUKUMU

Tunaamini kwamba wafu wadogo na wakubwa watafufuliwa na kusimama na walio hai mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu; na kwamba wakati huo kutatokea mgawanyiko wenye utisho wa Mungu ambapo waovu watahukumiwa katika adhabu ya milele na wenye haki watapata uzima milele; na kwamba hukumu hii itaweka hali ya watu mbinguni au jehanamu milele kwa kanuni za haki zilizoandika katika Neno Lake takatifu.

### Rejea ya Maandiko

Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya. 2 Wakorintho 5:10

Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, na kuwatupa katika tanuru ya moto, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao. Mwenye masikio, na asikie. Mathayo 13:41-43



## XIX. MBINGU

Tunaamini kwamba Mbingu ndio makao matukufu ya Mungu aliye hai; na kwamba huko Bwana ameenda kuandaa mahali kwa ajili ya watoto wake; na kwamba kaika jiji hili la mraba (foursquare), ambalo mjenzi wake na mwashi ni Mungu, waamini waaminifu ambao wameosha mavazi yao katika damu ya Mwana-Kondoo

na wameshinda kwa neno la ushuhuda wao watachukuliwa; kwamba Bwana Yesu Kristo atawawasilisha kwa Baba bila doa wala mkunjo wowote; na kwamba iko furaha isiyoeweza kutamkwa watakapoutazama uso Wake wa ajabu, katika ufalme wa milele usio kuwa na giza wala usiku, wala masikitiko, wala machozi, wala uchungu, wala mauti, na ambamo ndani yake majeshi ya malaika watumishi wakipiga vinubi vyao, na kuimba sifa za Mfalme wetu, na wakisujudu mbele ya kiti cha enzi, wakilia "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu."

## Rejea ya Maandiko

...Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. 1 Wakorintho 2:9

Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Yohana14:2

Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele. Ufunuo wa Yohana 22:5

Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita. Ufunuo wa Yohana 21:4

Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, na yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao. Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao. Ufuno wa Yohana 7:15-17



## XX. JEHENAMU

Tunaamini kwamba jehenamu ni mahali pa giza la nje na masikitiko makuu, ambapo mnyoo haifi na moto hauzimiki, mahali palipoandaliwa kwa ajili ya ibilisi na malaika zake, ambapo kutakuwepo na maombolezo kilio na kusaga meno, mahali pa mateso na majuto ya milele kwa wale ambao wamekataa rehema, upendo na huruma wa Mwokozi aliyesulubiwa, waliochagua mauti badala ya uhai, na kwamba katika ziwa liwakalo moto na kibeliti watatupwa wale wasio amini, wachukizao, wauaji, wachawi, wabuduo sanamu, na waongo wote, wale waliokataa na kusukumia mbali upendo na dhabihu ya Mkombozi avujae damu, wakipita msalabani na kwenda kwenye uharibifu wao, licha ya kuombwa sana na kuonywa na Roho Mtakatifu.

### Rejea ya Maandiko

Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, na kuwatupa katika tanuru ya moto, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. Mathayo 13:41-42

Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, alimo yule mnyama na yule nabii wa uongo. Nao watateswa mchana na usiku hata milele na milele... Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto. Ufunuo wa Yohana 20:10, 15

...yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake. Ufunuo wa Yohana 14:10-11

Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele,

aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake.. Mathayo 25:41

Na mkono wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili, na kwenda zako jehanum, kwenye moto usiozimika; ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki. Marko 9:43-44

Waambie, Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu; bali aghairi mtu mwovu, na kuiacha njia yake mbaya, akaishi. Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa, Enyi nyumba ya Israeli? Ezekieli 33:11



## XXI. UINJILISTI

Tunaamini kwamba baada ya kuona kwamba vitu hivi vyote vitaharibiwa na mwisho wa vitu vyote umekaribia, wana waliokombolewa wa Bwana Yehova watainuka na kuangaza kama nuru isiyoweza kufichika, mji uliojengwa juu ya kilima, wakipeleka injili kwa kasi hata miisho ya dunia, kuulinda ulimwengu na ujumbe wa wokovu, kutangaza kwa bidi ilioyowaka na kwa shauri lote la Mungu kwamba Bwana wa Utukufu atakapoonekana, wakutwe wamesimama, na viuno vyao vimefungwa na kweli, shughuli zao na huduma zielemewe na utajiri wa vito vya thamani ambavyo wameshinda na kutunza kwa ajili Yake, roho za thamani, ambazo, kwa ushuhuda wao wa uaminifu wametumika kama nyenzo katika kuongoza kutoka gizani kuja nuruni; kwamba kuziokoa roho ni shughuli kubwa zaidi za kanisa hapa duniani; na kwamba kila mzigo na kizuizi ambacho kinge jaribu kuzima miale au chochote ambacho kinaweza kufunika au kuzuia juhudi za kueneza au kufanya uinjilisti ulimwenguni kote inabidi kikatwe na kutupiliwa mbali kama kitu kisicho faa kwa kanisa,

kinachotaka kuleta uharibifu katika njia takatifu ya Kristo na ni kinyume na agizo kuu la Bwana.

## Rejea ya Maandiko

Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake; lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. 2 Timotheo 4:1-2

...mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu. Waefeso 5:16

...Na mwenye hekima huvuta roho za watu. Mithali 11:30

...jueni ya kuwa yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi. Yakobo 5:20

Mwanadamu, nimekuweka kuwa mlinzi wa nyumba ya Israeli; basi, sikia neno hili litokalo katika kinywa changu, ukawape maonyo haya yatokayo kwangu. Nimwambiapo mtu mbaya, Hakika utakufa; wewe usimpe maonyo, wala husemi na huyo mtu mbaya ili kumwonya, kusudi aache njia yake mbaya na kujiokoa roho yake; mtu yule mbaya atakufa katika uovu wake; lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Ezekieli 3:17-18

...Inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno. Naye avunaye hupokea mshahara, na kukusanya matunda kwa uzima wa milele, ili yeye apandaye na yeye avunaye wapate kufurahi pamoja. Kwa maana hapo neno hilo huwa kweli, Mmoja hupanda akavuna mwingine. Yohana 4:35-37

Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake. Mathayo 9:38

Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Marko 16:15

## XXII. ZAKA NA MATOLEO



Tunaamini kwamba njia iliyowekwa wakfu na Mungu kutegemeza huduma yake na kueneza injili baada ya agizo Lake ni "zaka" na inakubaliwa kwa ujumla katika makanisa yote ya Foursquare, siyo tu kama njia ya Mungu ya kutunza mahitaji ya vifaa nay a kifedha ya kanisa Lake, bali ni kuinua morali ya kiroho ya watu wake kiwango ambacho Mungu lazima awabariki. Tumeamiwa katika Malaki 3:10, "Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la." Katika swala la "utoaji" na "matoleo ya hiari," yameagizwa na Bwana na kutendewa kazi katika makanisa yote ya Foursquare kama sehemu ya mpango wa Mungu kwa mahitaji ya vifaa ya kanisa na ukiroho wa watu wake. Tumeshauriwa katika Luka 6:38, "Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa." Tukiwa "warithi pamoja Naye" tunajua kwamba kutoa katika ufalme Wake ambao ni wetu sisi ni kitu cha kufurahisha, kwa sababu heri kutoa kuliko kupokea, kwa kuwa tumeagizwa katika 2 Wakoritho 9:7, "Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu."

### Rejea ya Maandiko

Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa

kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja... 1 Wakorintho 16:1-2

Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Malaki 3:10

Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa. Luka 6:38

Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu. 2 Wakorintho 9:7

FMP

Foursquare Missions Press

© 2005